

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

**Dodoma
28 Machi, 2024**

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**RAIS SAMIA AAHIDI SERIKALI KUFANYIA KAZI RIPOTI ZA
CAG NA TAKUKURU**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameahidi kuwa Serikali itaifanyia kazi Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) pamoja na taarifa ya Utendaji Kazi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Pia ameahidi kuiwasilisha Bungeni ndani ya muda mfupi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa ripoti hizo zinasaidia kuimarisha utendaji kazi wa Serikali na Mashirika ya Umma pamoja na kujirekebisha.

Rais Samia amesema hayo wakati akizungumza na viongozi mbalimbali mara baada ya kupokea ripoti za taasisi hizo mbili za mwaka 2022/2023 Ikulu, Chamwino.

Licha ya kwamba ni takwa la kikatiba, Rais Samia amesema uwasilishaji wa Ripoti hiyo ni kuimarisha uwazi na uwajibikaji ambayo ni hatua ya awali kabla ya kusikia majibu ya Serikali kuhusu dosari zote zilizoainishwa.

Rais Samia amepongeza marekebisho yaliyofanyika kutokana na ripoti zilizopita kwani yamesaidia kupatikana kwa asilimia 99 ya hati safi na asilimia moja pekee ya hati chafu kwa kuwa ripoti hizo zinachagiza kuongezeka mapato.

Amesema dosari zilizotolewa zitafanyiwa kazi na Serikali na matumaini yake kuwa hazitajirudia katika ripoti zijazo.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu